

VURUGU NA UNYANYASAJI KAZINI HAUKUBALIWI

Watu wote wana haki ya kufanya kazi bila vurugu au unyanyasaji. Vurugu na unyanyasaji kazini havikubaliwi kamwe.



JE, VURUGU NA UNYANYASAJI KAZINI NI NINI?

Tabia ya mtu yeyote anayesababisha madhara, au anajaribu kusababisha madhara, kwa mtu mwingine au kwa kazi.

Mtu yeyote – wanawake na wanaume, wafanyakazi wenza, wakubwa, wasaidizi – anaweza kumfanyia vurugu au kumnyanyasa mtu mwingine kazini. Mifano ya kawaida ni pamoja na:



KIMWILI : Kupiga, au kutishia kumpiga mtu

KINGONO: Mawasiliano yasiokubalika au yanayoudhi, au kumgusa mtu mwili bila hiari yake.

KIAKILI : Kufedhehesha, uonevu au kutishia mtu kwa maneno au kitendo.

KIPESA: Kupunguzwa kwa mishahara, kunyimwa marupurupu

UNYANYASAJI WA KINGONO

Tabia ya kingono ambayo haimpendezi na inaudhi mtu kazini. Mtu yeyote – wanawake na wanaume, wafanyakazi wenza, wakubwa, wasaidizi – anaweza kumnyanyasa mtu mwingine kingono kazini au yeye kunyanyaswa. Mifano ya kawaida :



Kupiga miluzi na kushiriki nyenzo za kingono mahali pa kazi

Kuhitaji upendeleo wa kingono ili kutoa mkataba, ongezeko la mishahara, nk.

Simu, ujumbe, maneno ya kingono na yasiyopendeza.

JE, NI TABIA GANI ISIYO VURUGU AU UNYANYASAJI KAZINI?

Tabia ambayo HAIUDHURU au isiyojaribu kusababisha madhara. Tabia ambayo inafaa na HAIUDHI mtu anayeipitia kazini. Mifano ya kawaida :



Kugusana kimwili ambapo wahusika wote wanakubaliana bila shinikizo.

Kitendo cha mapenzi ambacho wahusika wote wanakubaliana kwa hiari.

Kufanya utani usiokera.

JINSI YA KURIPOTI VURUGU NA UNYANYASAJI KAZINI?

Vurugu na unyanyasaji kazini na unyanyasaji wa kingono huwadhuru watu na hudhuru biashara.

Ifichue, isuluhishe, ikomeshe!



Wasiliana na Kamati ya Malalamiko au Kamati ya Kutathmini-na-Kushughulikia au Kamati ya Jinsia au (weka hapa)

Wajumbe wa kamati yako ni :

Wasiliana na (piga simu/SMS) :